TANGAZO LA SERIKALI NA 837 la Tarehe 2/10/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA 288)

# SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 89

SHERIA NDOGO ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA, 2020

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za Mwaka 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa, hii ni pamoja na-

(a) kitu chochote kinacho tumika katika matengenezo ya chakula;
(b) kitu chochote kinacho ongeza ladha ya chakula;
(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari na vingine vinavyo

fanana na hivi);

“choo cha kuvuta” maana yake ni choo ambacho kimejengwa na kuunganishwa na maji na kuwa na tanki ya kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa uchafu hadi mahali palipo andaliwa;

“choo bora” maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwakwa vifaa vya kudumu, lenye vipimo vya futi 4 x 3 na kimo cha futi 12 na zaidi;

“choo cha umma” maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma;

“eneo la wazi” maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Mbeya;

“hati ya usafi” maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya;

“jengo la biashara” maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa;

“kaya” maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababishi-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;
(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi;
(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;
(d) magonjwa kwa binadamu,kuhifadhi mbu,nzi,panya na viumbe wenye madhara.

Sura 191

"kituo cha taka" maana yake ni kizimba cha taka kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri;

"maji taka"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"mmiliki" maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

Sura 191

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Sura 191

"mzalishaji wa taka ngumu" maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka;

"pipa la taka"maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

Sura 191

"taka"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191

"taka ngumu"maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka za majumbani" maana yake ni mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

"taka za viwandani" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ;

"uchafu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira;

"uchunguzi wa afya" maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;

"ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya nyumba, banda au zizi ndani ya eneo lililoruhusiwa na Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika lililoteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

## SEHEMU YA PILI

## USAFI WA MAZINGIRA

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki au anayeishi katika eneo la nyumba kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba;

(a) majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake;

(b) takataka ngumu na laini ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa nakupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Usafi wa mifereji ya maji ya mvua.

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa msafi na imara siku zote.

Usafi siku ya jumatano

6. Kila siku ya Jumatano itakuwa ni siku maalum ya ukaguzi wa jumla wa Usafi wa Mazingira ambapo wakaguzi kutoka Halmashauri watapita kufanya ukaguzi wa mazingira na itakapobainika kuwa mtu yeyote hajafanya usafi au kuna uchafuzi wowote katika eneo husika,

watachukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Usafi wa kila jumamosi

7 Kila Jumamosi ya Mwisho ya kila mwezi utafanyika Usafi wa Mazingira wa jumla kuanzia saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi, ambapo kila mtu au taasisi itawajibika kushiriki katika zoezi la Usafi wa Mazingira na wakati wote wa muda wa Usafi wa Mazingira shughuli zote zitasimamishwa isipokuwa huduma muhimu kama zitakavyoainishwa na Halmashauri.

Kupaka rangi majengo

8. Halmashauri itafanya uhamasishaji wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kwamba anapaka rangi nyumba yake au duka lake ndani na nje kila itakapochakaa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu.

9. Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo wa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Biashara ya miwa na matunda

10. Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ya matunda au miwa kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Upulizaji dawa

11. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinacho tambuliwa na Serikali na awe na leseni hai kutoka Halmashauri.

Matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo na kuegesha magari mabovu

12. (1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

## SEHEMU YA TATU

## UIMARISHAJI WA AFYA

Usalama wa maji ya kunywa.

13. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula.

14. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka kwa Bwana Afya wa Halmashauri.

Uuzaji vyakula vilivyopikwa.

15 Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Usalama wa vyakula.

16 Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza.

Uzuiaji wa shughuli

17. Afisa Mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile

mbalimbali wakati wa Magonjwa ya mlipuko

utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji wa vyombo vilivyotumika kuhifadhia chakula

18 (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata Vyakula, vyombo au vifaa vingine vyovyote vitakavyokuwa vinatumika mara baada ya kutolewa amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo vyakula vitakavyo kamatwa vitakuwa ni vile ambavyo vinaweza kuharibika kwa haraka Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuviharibu.

(3) Endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea endapo vyombo vitaharibika, isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Machinjio na maduka ya nyama

19. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba duka lake-

(a) ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu;
(b) lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama;
(c) lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani;
(d) lina pipa la kuhifadhia taka taka;.
(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na aproni

nyeupe; na

(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita

Kuchinja na kuuza nyama mahali pasiporuhusiwa

20 Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyo ruhusiwa na Halmashauri.

Uendeshaji wa biashara ya Nyumba za kulala wageni na Hosteli

21. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni na hosteli au nyumba za biashara kuhakisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla hajaanza biashara.

(2) Endapo mmiliki hajakidhi masharti ya kiafya Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya Nyumba za kulala wageni au hosteli mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba ya wageni na Hosteli

22. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, Hoteli na Hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika majengo hayo kuna-

(a) mwanga na hewa ya kutosha;
(b) nafasi na vifaa (samani ) za kutosha;
(c) uimara wa jengo;
(d) mfumo wa uondoshaji wa maji taka na taka ngumu wa kuaminika;
(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;
(f) vyoo na mabafu kwa jinsia zote;
(g) vifaa vya zima moto;
(h) tanki la kuhifadhia maji safi; na
(i) vyoo na bafu vilivyosakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita kutoka usawa wa sakafu.

Upimaji wa afya

23. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila Mmiliki wa hoteli, wafanyakazi wa machinjio, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari kupima afya kila baada ya miezi sita na watalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5,000/=).

(2) Mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atalazimika kupima afya kila baada ya miezi sita na atalipa ada ya upimaji wa afya kiasi cha shilingi elfu tano (Tsh.5,000/=).

(3) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake atakuwa ametenda kosa.

Uwezo wa kukagua

24. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wakati wa saa za kazi kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya

25. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Ada ya ukaguzi wa afya

26. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kulipa ada

27. (1) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwanzo wa mwaka wa fedha wa Halmashauri yaani mwezi Julai.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kulipa ada katika kipindi cha miezi miwili baada ya mwaka wa fedha kuanza atawajibika kulipa kiwango hicho pamoja na adhabu ya asilimia hamsini ya kiwango anachodaiwa.

## SEHEMU YA NNE

## UZOAJI TAKA

Kuweka eneo katika hali ya

28. Kila mwenye nyumba au eneo au mtu mwenye dhamana ya nyumba au eneo anatakiwa kuweka

usafi

mazingira ya nyumba au eneo lake katika hali ya usafi wakati wote na kuhakikisha hakuna taka zinazotupwa katika eneo lake.

Taka kutupwa kwenye gari la taka

29. Kila kaya au wapangaji katika nyumba au wafanyabiashara watakuwa na jukumu la kutunza, kubeba na kupeleka taka walizozizalisha na kuzitupa moja kwa moja kwenye gari la kubeba taka kwa kuzingatia ratiba na utaratibu uliowekwa na Halmashauri au kuzitupa katika makasha ya taka (Skip buckets) yaliyowekwa katika baadhi ya maeneo.

Jukumu la kuwa na chombo cha kuhifadhia taka

30 Kila mwenye nyumba au mpangaji, mmiliki au msimamizi wa eneo la biashara, taasisi na ofisi ndani ya Halmashauri anatakiwa awe na pipa dogo au ndoo au chombo au kifaa chochote chenye mfuniko yaani “waste bins”kwa ajili ya kuhifadhia taka zinazozalishwa katika eneo hilo kwa ajili ya madhumuni yaliyotajwa.

Wajibu wa mmiliki wa chombo cha usafiri

31 (1) Mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri wa umma anawajibika kuweka chombo au kifaa cha kuhifadhia taka kwa ajili ya abiria wake.

(2) Kila mmiliki au dereva wa chombo cha kusafirishia mizigo, taka au madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha anaweka vifaa vya kufunika bidhaa anazosafirisha ili kutoruhusu bidhaa hizo kudondoka au kumwagika na kuchafua mazingira.

marufuku

32 Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa hovyo vitu kama vile vocha ya simu iliyokwisha kutumika, maganda ya muwa, majani ya mahindi, magunzi, chupa za vinywaji au kitu chochote kinachoweza kuchafua mazingira mahali ambapo siyo kwenye chombo cha takataka au siyo rasmi kwa kutupwa takataka.

Ada ya uzoaji taka

33. (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kutoka kwa kila kaya au mwenye jengo la biashara kwa viwangovilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri itatoza gharama za utupaji wa taka katika dampo lililoko Nsalaga kutoka kwa mawakala, wamiliki wa taasisi mbalimbali, viwanda na makampuni pamoja na wazalishaji wengine wa taka kwa viwango vilivyoainishwa katika jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

(3) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa afisa mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(4) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii (CBOs)

34. (1) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi vya kijamii (CBOs) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

(2) Majukumu mahsusi ya vikundi vitakavyoundwa katika kifungu kidogo cha (1)yatakuwa ni-

(a) kukusanya, kuzoa na kusafirisha taka kutoka maeneo yote ya uzalishaji na kuzipeleka katika dampo kuu la Halmashauri lililopo Nsalaga; na

(b) kukusanya ada ya Usafishaji na uondoshaji taka katika maeneo ya makazi na biashara na kuwasilisha kiasi kilichokusanywa kwenye mfuko wa mazingira wa Kata husika ambapo 70% ya mapato ya ada itatumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za usafi za kikundi husika na 20% itabaki kwa ajili

ya matumizi ya uendeshaji wa shughuli za Dampo la kisasa na 10% itabaki kwa ajili shughuli za Ofisi ya Kata na mitaa husika.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

35. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kwenda kutupwa.

Kutupa taka katika sehemu maalum

36. Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Marufuku kutupa taka hovyo

37. Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa taka, uchafu wowote au kuacha kuwepo takataka mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.

Uhifadhi maji taka

38. Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

Kutiririsha maji taka

39. Ni marufuku kutiririsha au kuelekeza maji kutoka vyooni, bafuni,karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka.

Taka za viwanda

40. (1) Itakuwa ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai.

Uteuzi wa wakala

41. Halmashauri inaweza kuteua kampuni, kikundi, kikundi cha jamii au Mtu binafsi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

**SEHEMU YA TANO**

**UJENZI NA MATUMIZI YA VYOO**

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

42. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.

Umbali wa kujenga choo

43. Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa zaidi ya mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya Nyumbani.

Vyoo vya umma

44. (1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au Taasisi kujenga vyoo vya Umma (Public toilet) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawalaka watakaopewa kusimamia vyoo hivyo.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

45. Itakuwa ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya ujenzi, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri

Vyoo katika majengo ya biashara

46. Kila mmiliki wajengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo viwili vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa

ajili ya matumizi ya wateja wake wa jinsia zote.

Ilani ya kujenga choo

47. Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hizi.

Ilani ya kuondoa kero

48. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Halmashauri kuteua mkaguzi

49. Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi katika eneo la Halmashauri.

Uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo

50. Chini ya Sheria Ndogo hizi Mkaguzi atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira kwa kutupa takataka mahali popote pasiporuhusiwa ilimradi kuwa adhabu hiyo izingatie masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Makosa

51. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo-

(a) atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;
(c) atamwaga takataka barabarani au katika

mtaro wa maji ya mvua au uchochoroni au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;

(f) ataosha magari au kufua au kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo cha maji au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(g) atauza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo mengine;

(h) atafanya matengenezo ya magari au pikipiki au mitambo au kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(i) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba ya makazi au maeneo yasiyoruhusiwa;

(j) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni au upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni;

(k) atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

Adhabu

52. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufililisha kosa

53 Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini

isiyozidi shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoelekezwa katika Jedwali la Sita la Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

(limetungwa Chini ya kifungu cha (26)

Ada ya ukaguzi wa Afya

| Na. | **Aina ya biashara** | **Ada kwa mwaka** |
|---|---|---|
| 1. | Baa na maduka ya vinywaji (Groceries) | 10,000/= |
| 2. | Migahawa /mama lishe | 10,000/= |
| 3. | Nyumba za wageni (Guest House) na Hoteli | 10,000/= |
| 4. | Kumbi za starehe au mikutano | 10,000/= |
| 5. | Hotel | 100,000/= |
| 6 | Kiwanda | 100,000/= |
| 5. | Majengo mengine ya biashara | 10,000/= |

## JEDWALI LA PILI

(Limetungwa chini ya kifungu cha 33)

ADA YA TAKA KWA KAYA, BIASHARA NA TAASISI

| **No** | **AINA YA ADA YA TAKA** | **ADA KWA MWEZI** |
|---|---|---|
| 1 | Kaya | 2,000/= |
| 2 | Mgahawa | 20,000/= |
| 3 | Nyumba ya kulala wageni | 10,000/= |
| 4 | Zahanati ( Taka zisizo hatarishi) | 20,000/= |
| 6 | Kituo cha afya (Taka zisizo hatarishi ) | 50,000/= |
| 7 | Hospitali ya Rufaa (Taka zisizo hatarishi) | 500,000/= |
| 8 | Hospitali (Taka zisizo hatarishi) | 200,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Kiwanda cha mbao | 20,000/= |
| 10 | Fundi seremala | 5,000/= |
| 11 | Huduma za uchomeleaji | 15,000/= |
| 12 | Karakana nyinginezo | 20,000/= |
| 13 | Kiwanda kidogo | 50,000/= |
| 14 | Kiwanda kikubwa | 300,000/= |
| 15 | Duka la jumla | 20,000/= |
| 16 | Duka la rejareja/huduma | 5,000/= |
| 17 | Shule ya msingi ya bweni | 100,000/= |
| 18 | Shule ya sekondari ya bweni | 100,000/= |
| 19 | Kituo cha kulelea watoto | - |
| 20 | Duka dogo la chakula | 5,000/= |
| 21 | Duka kubwa la chakula | 30,000/= |
| 22 | Baa | 20,000/= |
| 23 | Klabu za usiku | 100,000/= |
| 24 | Kituo cha burudani/kumbi za starehe/na sherehe | 100,000/= |
| 25 | Duka la nyama na samaki | 10,000/= |
| 26 | Nyama choma/chips inayojitegemea | 5,000/= |
| 27 | Duka la dawa la jumla na rejareja | 25,000/= |
| 28 | Duka la dawa la rejareja | 10,000/= |
| 30 | Dobi mdogo (mikono) | 2000/= |
| 31 | Dobi mkubwa (Laundry) | 10,000/= |
| 32 | Fundi vifaa vya umeme | 5,000/= |
| 33 | Fundi kushona kwa kila cherehani | 2000/= |
| 34 | Kutengeneza nywele/saluni | 10,000/= |
| 35 | Kituo cha kuuza mafuta na vilainishi vya magari na mitambo | 50,000/= |
| 36 | Stoo mbalimbali | 5,000/= |
| 37 | Ghala | 50,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 38 | Hoteli | 100,000/= |
| 39 | Taasisi kubwa (Taasisi kubwa za kifedha) | 100,000/= |
| 40 | Taasisi Ndogo (Taasisi ndogo za kifedha) | 50,000/= |
| 41 | Kilabu ya pombe ya kienyeji | 3,000/= |
| 42 | Kituo cha kulaza wageni(Hostel) | 100,000/= |
| 43 | Kituo cha mazoezi ya viungo (Gym) | 10,000/= |
| 44 | Kiwanja cha michezo | 20,000/= |
| 45 | Fundi viatu | 2,000/= |
| 46 | Stoo ya mkaa | 10,000/= |
| 47 | Mama/Baba lishe | 5,000/= |
| 48 | Duka la kuuza magari | 30,000/= |
| 49 | Duka la madawa ya mifugo na zana za kilimo/pembejeo jumla | 25,000/= |
| 50 | Duka la madawa ya mifugo na zana za kilimo/pembejeo rejareja | 10,000/= |
| 51 | Studio ya picha | 10,000/= |
| 52 | Maeneo ya kuuza mbao (timber yard) | 15,000/= |
| 53 | Duka la mitambo na mashine | 10,000/= |
| 54 | Mashine ya kukoboa na kusaga nafaka | 10,000/= |
| 55 | Mashine ya kukamua mafuta | 20,000/= |
| 56 | Kiwanda cha mikate | 50,000/= |
| 57 | Duka la shajala | 10,000/= |
| 58 | Duka la vifaa vya ujenzi (Hardware) | 20,000/= |
| 59 | Ofisi ya kampuni/Ushauri | 10,000/= |
| 60 | Duka la mawakala wa fedha | 5,000/= |
| 61 | Wauza bidhaa mbalimbali sokoni | 2,000/= |
| 62 | Duka la pikipiki na baiskeli | 10,000/= |
| 63 | Vituo vya boda boda | 5,000/= |
| 64 | Duka la kuuza vipuri (spare) dogo | 5,000/= |
| 65 | Duka la kuuza vipuri (spare) kubwa | 10,000/= |

## JEDWALI LA TATU

*Limetungwa chini ya Kifungu cha 33(2))*

Gharama za utupaji wa taka katika jaa la taka la Halmashauri

| NA. | AINA YA TAKA | KIASI CHA TAKA | KIWANGO |
|---|---|---|---|
| 1. | Taka za nyumbani | Zaidi ya tani moja<br>Chini ya tani moja | 50,000/=<br>40,000/= |
| 2. | Taka za viwandani | Zaidi ya tani moja<br>Chini ya tani moja | 70,000/=<br>50,000/= |
| 3. | Taka hatarishi | Zaidi ya tani moja<br>Chini ya tani moja | 100,000/=<br>80,000/= |

## JEDWALI LA NNE

*(Limetungwa Chini ya kifungu cha 47)*

## ILANI YA KUJENGA CHOO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha (45) cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya, 2020.

**SEHEMU 'A'**

Ndugu…………............wa Mtaa/Kijiji……………….…Kata ya…………………
Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika
Tarehe……mwezi………..mwaka….
Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma*/ Namba…………
iliyopo eneo la ………………katika Kitongoji/Mtaa*……….Kijiji
cha……………Kata ya………….
Imekuwa haina choo/ choo kimejaa/kimeharibika* hivyo unaamriwa kutekeleza mambo yafuatayo;

(1) ………………………………………………………………………………
(2) ………………………………………………………………………………
(3) ………………………………………………………………………………
(4) ………………………………………………………………………………

SEHEMU 'B'

Unapewa muda wa siku thelathini (30) tu tangu siku ya kupokea ilani hii kutekeleza maelekezo yote yaliyoelezwa katika sehemu 'A' ya Ilani hii,

SEHEMU 'C'
Ukaguzi wa kuthibitisha utekelezaji wa maelekezo uliyopewa utafanyika tarehe……………….endepo utashindwa kutekeleza maelekezo ndani ya muda uliopewa Halmashauri itakuchukulia hatua kali za kisheria bila kukupa taarifa nyingine.

………………………………..
AFISA MWIDHINIWA

IMETOLEWA NA; IMEPOKELEWA NA;
Jina;……………………….Jina;………………………………….
Saini………………………
saini……………………………….....
Wadhifa…………………...
wadhifa……………………………..
Tarehe……………………..
Tarehe……………………………...

*Futa lisilotakiwa.

JEDWALI LA TANO

*Limetungwa Chini ya kifungu cha 48*

ILANI YA KUONDOA KERO

Ilani hii imetolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 47 cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

SEHEMU 'A'
Ndugu…………………........wa Mtaa/Kijiji……………Kata ya…………………
Unaarifiwa kwamba katika ukaguzi uliofanyika
Tarehe……mwezi………..mwaka….
Katika nyumba yako ya Biashara/kuishi/kutolea Huduma/kiwanja* iliyopo eneo la………………………………………………………………………………
…..kumekutwa machukizo/kero/uchafu*; kama ifuatavyo;

1) ……………………………………………………………………………
2) ……………………………………………………………………………
3) ……………………………………………………………………………
4) ……………………………………………………………………………

SEHEMU 'B'
Kwa ilani hii unaamriwa kurekebisha/kuondoa/kusafisha* kwa;

1. ……………………………………………………………………………
2. ……………………………………………………………………………

3. ………………………………………………………………………………
4. ………………………………………………………………………………

SEHEMU ‘C’
Unapewa muda wa siku saba (7) tangu siku ya kupokea ilani hii, unatakiwa kutekeleza yote yaliyoelezwa katika sehemu ‘B’ ya Ilani hii, kushindwa kwako kutekeleza ndani ya muda uliopewa Halmashauri italazimika kukuchukulia hatua kali za kisheria bila kulazimika kukupa taarifa nyingine.

……………………………..
AFISA MWIDHINIWA

IMETOLEWA NA; IMEPOKELEWA NA;
Jina;……………………….Jina;………………………………….
Saini………………………
saini………………………………....
Wadhifa…………………...
wadhifa……………………………..
Tarehe……………………..
Tarehe……………………………...

*Futa lisilohusika

JEDWALI LA SITA
(*Limetungwa* c*hini ya Kifungu cha 53*)
HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi ………………………………………………… nakiri mbele ya ……………………………………… ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi ninachodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe …… ya mwezi …………… mwaka …………
Jina……………………..…………………………

Saini……………

Mbele ya:
Jina………………………………………………….
Cheo ……………………………………………..
Saini ………………

Muhuri wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio la kikao cha Mkuatano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10/06/2020 na kubandikwa mbele ya;

SAAD A. MTAMBULE
*Kaimu Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**LS**

GIBSON J. MWAKALIBULE
*Mwenyekiti wa Mkutano*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**NAKUBALI**

DODOMA
05 Agosti, 2020

SELEMANI S. JAFO
WN OR-TAMISEMI
DODOMA